

BWANA NDIYE FUNGU LA POSHO LANGU

Zaburi ya Katikati

Dominika ya 13 ya Mwaka C

$\text{♩} = 70$

Bwa - na ndi - ye fu - ngu la po - sho la - ngu.

Bwa - na ndi - ye fu - ngu la po - sho la - ngu.

Mashairi

Mu - ngu uni - hi - fa - dhi mi - - mi, kwa maana naku - ki - mbi - li - a we - we.

Ni - me mwambia Bwana, Ndi - we Bwa - na wa - ngu; Bwa - na ndiye fungu la po - sho la - ngu.

Na la ki - ko - - mbe cha - ngu; We - we u - na - i - shi - ka ku - ra ya - ngu.

2. Nitamhimidi Bwana aliyenipa shauri,
Naam, mtima wangu umenifundisha usiku.
Nimemweka Bwana mbele yangu daima,
Kwa kuwa yako kuumeni kwangu, sitaondosha.

3. Kwa hiyo moyo wangu unafurahi,
na utukufu wangu unashangilia,
Naam, mwili wangu nao utakaa kwa kutumaini.
Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu,
wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu.

4. Utanijulisha njia ya uzima;
mbele za uso wako ziko furaha tele;
na katika mkono wako wa kuume
mna mema ya milele.